**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA SABA

## KIKAO CHA TATU

**07 NOVEMBA, 2019**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA SABA

## KIKAO CHA TATU – TAREHE 07 NOVEMBA, 2019

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**30. MHESHIMIWA EZEKIEL MAGOLYO MAIGE (MSALALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Wananchi wa Msalala kwa juhudi zao wamejenga Mabweni katika Shule za Sekondari za Bulige, Busangi, Baloha, Mwalimu Nyerere, Lunguya, Ntobo na Isaka:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kuunga mkono juhudi hizo za Wananchi kwa kuyatambua Mabweni hayo na kuzipatia Shule hizo ruzuku za uendeshaji wa Mabweni kwa ajili ya umeme, maji, chakula na ulinzi;

(b) Je, Serikali ipo tayari kuongeza miundombinu kama mabwalo ya chakula na nyumba za *matron* katika Shule hizo;

(c) Je, ni lini Serikali itasaidia Wasichana wa Msalala katika Kata zingine kama Mwanase, Mwalugulu, Jana, Bugerema na Bulyanhulu kwa kuwajengea Mabweni.

**31. MHESHIMIWA MASOUD ABDALLAH SALIM (MTAMBILE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji unatarajiwa kufanyika mwezi Novemba, 2019:-

Je, Serikali inasema nini juu ya ushirikishwaji wa Vyama vya Siasa katika Mkakati wa kutoa elimu ili kufikia lengo la Uchaguzi huru na haki.

**32. MHESHIMIWA ROSE KAMIL SUKUM (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mpango wa Serikali kupeleka fedha za afya moja kwa moja kwenye Vituo vya kutolea huduma za Afya umesaidia kupunguza changamoto ya upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na stahiki za Watumishi. Lakini Waganga Wafawidhi hufanya kazi za Wahasibu

na Maafisa Manunuzi na hivyo kusababisha kutotoa huduma kwa Wagonjwa kwa wakati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka kuajiri Wahasibu na Maafisa Manunuzi kwa kila Zahanati.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**33. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (B.L.W):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):- Kwa mujibu wa taarifa ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya mwaka 2014, Kisiwa cha Latham ni mali ya Zanzibar tangu kilipofunguliwa rasmi mwaka 1898; Hata hivyo zipo taarifa zilizothibitishwa kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu iliiandikia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuwaarifu kuwa Kisiwa hicho ni cha Tanzania Bara:-

(a) Je, ni lini Serikali hizi mbili ambazo ni ndugu wa damu watakaa kutatua kero hii ya muda mrefu;

(b) Je, Serikali haioni kuwa umefika muda muafaka kulifanyia kazi suala hilo.

**34. MHESHIMIWA FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):- Kwa kuwa Muungano wetu ni tunu na tunahitaji kuwatunza hata Wazee wetu wanne walioshiriki kuchanganya mchanga wa Muungano wetu baina ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar:-

(a) Je, Serikali inawaangalia vipi Wazee wetu hao wanne kwa kuwapa asante baada ya utu uzima kuwafika;

(b) Wakati wa Sherehe za Muungano, Wazee hao hufikishwa kwenye Sherehe; Je, huko ndio kuonesha Serikali inawatunza.

## WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

**35. MHESHIMIWA AIDA JOSEPH KHENAN (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:- Je, ni lini Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) litajenga nyumba za bei nafuu ambazo Wananchi wenye hali ya chini wataweza kununua.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**36. MHESHIMIWA JUMA OTHMAN HIJA (TUMBATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Kumekuwa na usikivu hafifu wa mawasiliano katika baadhi ya Visiwa vidogo hapa nchini kama vile kisiwa kidogo cha Tumbatu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo hilo.

**37. MHESHIMIWA MARTHA JACHI UMBULLA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Uwanja wa Ndege wa Arusha ni muhimu sana kutokana na ukweli kuwa ni lango la kurahisisha Watalii kuelekea kwenye Mbuga zetu za Wanyama na Hifadhi za Taifa:-

(a) Je, ni lini Serikali itapanua na kuboresha uwanja huo ili kuwezesha Watalii wengi kutumia ndege zetu na nyingine kutua Arusha kwa urahisi;

(b) Je, Serikali haioni kuwa Uwanja wa Ndege wa Arusha ungetumika kimkakati kukuza Sekta ya Utalii nchini na kuongeza pato la Taifa.

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**38. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:- TBC hutangaza habari na vipindi mbalimbali kwa lugha ya Kiswahili ili Watanzania wasikie; Tanzania pia ina wageni kutoka nchi mbalimbali duniani waishio nchini, lakini TBC imekuwa ikitangaza taarifa za Habari na vipindi vyake vingine kwa Lugha ya Kiswahili tu; zamani kulikuwa na kipindi cha *External Service* kilichokuwa kikitangazwa kwa lugha ya Kiingereza ili wageni waishio nchini wasikie lakini sasa hivi hakipo:-

(a) Je, ni kwa nini TBC ilifuta kipindi cha *External Service* kilichokuwa kikitangaza taarifa ya habari kwa Lugha ya Kiingereza;

(b) Je, kwa kutangaza taarifa ya habari kwa Kiswahili tu hatuoni kwamba tunawanyima wageni fursa ya kujua kinachoendelea nchini.

**WIZARA YA KILIMO:**

**39. MHESHIMIWA BALOZI ADADI MOHAMED RAJAB (MUHEZA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Wananchi wa Tarafa ya Amani wamelima zao la Pilipili manga kwa wingi, hivi karibuni bei ya zao hilo imeanguka sana kutoka 12,000/= hadi 4,000/= jambo linalowaumiza sana Wakulima:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutuma Wataalam kubaini ni kwa nini zao hilo limeshuka thamani;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia Wakulima hao ili walime kilimo cha kisasa.

## III. KAMATI YA MIPANGO:

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

***(Majadiliano yanaendelea)***

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **S. KAGAIGAI** |
| **07 NOVEMBA, 2019** | **KATIBU WA BUNGE** |